

THE STATE UNIVERSITY
OF ZANZIBAR

P.O. Box 146

Tel: 255-242230724/2233337

Zanzibar – Tanzania

Fax: 255-24-2233337

E-mail: vc@suza.ac.tz

Web site: www.suza.ac.tz



CHUO KIKUU CHA TAIFA
CHA ZANZIBAR

S.L.P 146

Simu: 255-24-2230724/2233337

Zanzibar - Tanzania

Fax: 255-24-2233337

E-mail : vc@suza.ac.tz

Web site: www.suza.ac.tz

27 Mei, 2020

**TANGAZO KWA WANAJUMUIYA WOTE WA CHUO KIKUU CHA TAIFA
CHA ZANZIBAR (SUZA) KUHUSU KUFUNGULIWA KWA SHUGHULI ZA
ZA MASOMO YA VYUO VIKUU BAADA YA HALI YA UGONJWA WA
VIRUSI VYA CORONA (COVID-19) KUTENGEMAA**

Kutokana na agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli la kuruhusu kufunguliwa kwa **Vyuo Vikuu** ifikapo tarehe **1 Juni, 2020** pia agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la tarehe 27 Mei, 2020 kupitia kwa Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinawaarifu wanafunzi wake katika Kampasi zote kuhudhuria Chuoni kwa ajii ya kuendelea na masomo ya semesta ya pili kuanzia tarehe iliyotajwa.

Mambo yafuatayo yanatakiwa kufanywa na wanafunzi watakapofika Chuoni:

- i. Kukamilisha taratibu za malipo kwa semesta ya pili na kusawazisha tofauti ya malipo kwa wale wote walioshindwa kukamilisha malipo kwa semesta iliyomalizika.
- ii. Kuchukuwa hatua mbali mbali za tahadhari kujikinga na Covid-19.
- iii. Kufuatilia kwa karibu sana kupitia katika tovuti ya Chuo na mbao za matangazo katika Kampasi zote masuala yote kuhusu jinsi gani uendeshaji wa masomo hayo utakavyofanyika mara tu baada ya kuripoti Chuoni.

Kwa tangazo hili, wanataaluma wote walioko likizo wanatakiwa kuripoti kazini kuanzia tarehe 28 Mei, 2020 ili kuendelea na shughuli za kitaaluma.

Aidha Wanajumuiya wote wanaagizwa kuendelea kuchukuwa tahadhari na kufuata maagizo yote yaliyotolewa na yatakayotolewa na Serikali pamoja na wataalamu wa afya kuhusiana na kujikinga na uwezekano wa kuenea kwa maambukizi ya maradhi haya thakili.

Dkt. Zakia Mohammed Abubakar
Makamu Mkuu wa Chuo

